

Kwenda
Kambi na
Watoto



Ni wakati wa kwenda kambi!

Napenda kwenda katika kambi! Inavutia sana kuwa katika misitu, kulala chini ya nyota na kuvuta hewa ya kiasili. Ni ya ajabu kuweza kunywa kutoka kwenye asili, lakini ukweli ni kwamba kuwapeleka watoto kambini mara nyingi kunaweza kusababisha mabadiliko makubwa katika maisha yao. Tunawaondoa kutoka kwa kila kitu wanachojua na kuwasaidia kushiriki na Mungu. Hakuna chochote cha kulinganisha nacho.

Nikiwa mtoto nilifanya ahadi nyingi kwa Mungu nikiwa katika baadhi ya kambi kila mwaka, na najua kwamba Mungu alinisikia. Nilipata nafasi ya kwenda katika kambi pamoja na Kanisa langu kwa sababu walinizawadi kwa kujua fungu za Biblia. Kila mwaka nilitia bidii na kupata fursa yangu kwenye kambi! Nawashukuru sana walimu na viongozi walionisaidia na kuwekeza katika maisha yangu, wale walionisaidia kwenda kambi na wale walionihudumia katika kambi.

Ningependa kukuhimiza ufanye jitihada na kupanga kwenda kwenye asili pamoja na darasa lako. Wapeleke mahali fulani maalum; na ikiwa utaweza, kaa nao kwa usiku mmoja. Panga vitu vya kujifurahisha, chakula na kushiriki nao kuhusu Mungu. Unafahamu kwamba itachukua jitihada, kupanga, fedha na usumbufu. (Sitaki tena kulala chini!) Lakini bila shaka, unajua kwamba ina faida yake!

Hapa kuna kidokezo kabla ya kwenda katika kambi na darasa lako; jaribu kurudi nyumbani na kiasi sawa cha watoto.




Furaha ya Matembezi,

Dada Kristina Krauss

Jedwali la yaliyomo

Uongozi.....	3-4
Matembezi ya Asili.....	5-6
Ufundi.....	7-8
Vyakula.....	9-10
Usalama.....	11-12
Ziada.....	13-14



1. Kusajili



Wewe binafsi waalike watoto kwenye kambi: “Nataka WEWE uende NAMI katika kambi.” Shirikisha wengine, waombe waalike marafiki zao wote kambini pia. Uliza mapema, uliza mara kwa mara, uliza kila mtu na uulize tena. Kwa mfano, kiongozi alimwalika mtoto kambini mara kadhaa, na mara ya kumi na tatu, mvulana akaitikia, alikwenda kambini na huko akamkubali

Kristo! Usiwe mjeuri, lakini usife moyo. Muda mrefu wakiwa mbali na utaratibu wao wa kila siku unaweza kuwafanya watoto wawe na hisia zaidi kwa Bwana na kuleta mabadiliko makubwa katika maisha yao ... hivyo endelea kuwashawishi watoto hao kwenda kambini!

2. Kuongoza makundi madogo

Ni wajibu wetu kutengeneza mazingira inayowafanya watoto kushiriki, kuzungumza na kufikiria. Usiri LAZIMA uwepo; hivyo, kumbusha kila mtu kuwa kile kinachosemwa kambini kinabaki kambini. Kuwa na wakati wa “kuvunja barafu” ambao utasaidia watoto kujuana wenyewe na kujua kiongozi wao.

Uliza maswali bora yasiyo na majibu ya “Ndiyo au Hapana”. Badala ya kuuliza “Je, umefurahia leo?” Uliza, “Ni sehemu gani nzuri zaidi ya siku kwako?” Viongozi wengi huzungumza sana wakiwa

na makundi madogo katika kambi. Waache watoto waweze kuzungumza. Ili mazungumzo yaendeleo vyema, watie moyo watoto mara kwa mara, jua udhaifu wako, na jibu maswali kwa kuuliza maswali zaidi! Unapouliza swali ambalo unatarajia majibu kutoka kwa kila mtu, njia ambayo wakati mwingine hufanya kazi ni kuwa na kitu kinachorushwa, kwa mfano: mfano wa nyama au soksi chafu.

Kitu chochote utapata chini kitaweza kutumika. Mtu aliye na kitu hicho mkononi mwake atachagua mtu atakayefuata kuzungumza na kumtupia kitu hicho. Hata hivyo, watoto wana haki ya kubaki kimya. Wanapokea kitu na kusema “Anayefuata” na kutupa kitu kwa mtu anayefuata kuzungumza. Kwa njia hiyo, watakuwa na fursa ya kushiriki, lakini si lazima kushiriki. Tunapowafanya wanafunzi wajihisi sawa zaidi, ndivyo watakvayofungua mioyo yao zaidi na kupokea kile tumewaandalia katika kambi!



Uongozi

3. Kuwapa Maono



Viongozi wa vikundi katika kambi ndio sehemu muhimu zaidi ya programu. Amini usiamini, chochote kinachoendelea kambini na mpango wowote wa safari uliopo ni kuwawezesha viongozi wa vikundi vidogo kuwa

na majadiliano na watoto, ambapo wanahimizwa kuwa na uhusiano wa kibinafsi na Yesu Kristo. Wakati mwingine inaweza kuonekana kana kwamba wasimamizi wa programu, wasimamizi wa sherehe, au wanamuziki ndio watu muhimu zaidi kambini. Lakini sifa zao ni za muda tu, lakini urafiki tunaotengeneza na watoto sio. Viongozi wa makundi madogo watarudi nyumbani na wanafunzi wao na wanaweza kuwasiliana nao kwa miaka mingi. Hakikisha viongozi wako wanafahamu umuhimu wa jukumu lao kambini.

4. Kumwongoza mtoto kwa Kristo

Wanapohisi kwamba mtoto yuko tayari, ni muhimu kwa viongozi wako kuwa tayari kuuliza swali “Ungependa kuwa na uhusiano wa kibinafsi na Yesu?” au “Je! Ungependa kuwa Mkristo?”

Hapa kuna mfano wa sala:

“Baba, ni fursa kuu kuweza kuzungumza nawe leo! Nina mmoja ambaye ningetaka kukueleza.

_____, mtoto wako aliyepotea, ambaye sasa anarudi kwako! Wamegundua kuwa kuishi maisha bila wewe siyyo inavyostahili kuwa. Wao wamebadilika, kutoka kwa njia yao ya zamani ya kufikiri na ya kuishi, na wameanza kutembea wakikukaribia Baba wa mbinguni. Asante kwa kuwasamehe. Asante kwa kukimbia kuwapokea wanaporudi nyumbani. Tunatarajia mema kwa kila kitu utakachotenda na kwa mtoto huyu aliyerudi nyumbani. Na tunajua kwamba jambo la kwanza utakalotenda ni kuwa na karamu kuu mbinguni usiku wa leo kusherehekea. Tutasherehekea pia! Asante tena, Baba, kwa kukaribisha _____ nyumbani kwa mikono wazi. Tunatarajia kuwa utawawezesha kujua maana ya kuishi nao nyumbani. Amina.”

Baada ya kuongoza mtu kwa Bwana, endelea kuwa na mawasiliano ya karibu nao, na kuwasaidia kueleza wengine kuhusu kile kilichotokea. Zungumza nao kuhusu uwezekano wa kushiriki na kila mtu mwishoni mwa wiki jinsi walivyompokea Kristo na jinsi walivyo sasa kama Mkristo. Zungumza nao kuhusu maisha yao watakaporudi nyumbani, na kama unaweza wakabidhi vifaa vya kufuatilia au Agano Jipya.



5. Matembezi ya Kumbukumbu

Chagua vitu 10 ambavyo vinahusiana na mazingira ya kambi au matembezi kama vile: sonobari, mbegu, jiwe, tawi refu, tawi la miiba, jani la mti, kipande cha mbaao kwa ajili ya moto, n.k (Hadi vitu 10.)

Weka vitu hivyo chini ya kitu na kuzifunika, koti, shati, blanketi au hata kitambaa.

Kisha pamoja na wanakambi wako

wanaokuzunguka, funua vitu na uwaache watoto waziangalie kwa sekunde 5 hadi 10.

Tuma wanakambi wako kutafuta vitu vinavyofanana karibu na kambi au njiani. Weka muda wa dakika 5 hadi 15. Wanakambi wachanga wanapaswa kwenda kwa jozi, kumbuka usalama wa “Mfumo wa Rafiki.” Mwanakambi au wanakambi watakaorudi na vitu vingi watashinda.



6. Matembezi ya Asili




Kuwa na muda kwa watoto kwenda msituni au bustani ambapo ni salama, isiyo na kelele na ya kuvutia, ili waweze kuwa na wakati wa kutafakari tu maua, kusikiliza sauti, kulala chini kwenye nyasi, n.k. Waache watafute kitu cha kuwaza kwa muda na kumshukuru au kuzungumza na Mungu kuhusu hilo. Baada ya muda, rudi na kuwahimiza watoto wengine washiriki mambo haya na kundi nzima. Unaweza pia kula chakula cha mchana kwa pamoja kwenye misitu, au unaweza kutafuta njia za wanyama. (Kwa furaha zaidi, viongozi wanaweza kutengeneza njia maalum mapema, hivyo watoto wanaweza kuzitafuta.)

Matembezi

7. Matembezi ya Mawindo ya Mkangaji

Kila timu inapewa orodha ya vitu inavyopaswa kukusanya kutoka asilini. Timu zote zina orodha sawa. Hakikisha wanaenda angalau kwa jozi na kuweka mipaka mapema ya umbali watapofika. Hapa kuna vidokezo vya kile unaweza kuweka kwenye orodha:

- * Tunda
- * Jani
- * Kitu kikubwa kuliko kiatu
- * Kitu cha laini upande mmoja na mkwaruzo kwa upande mwingine
- * Mabaki ya ustaarabu
- * Kitu kwa ajili ya zawadi
- * Kitu chembamba na kirefu
- * Kitu kwa ajili ya kiongozi wao
- * Jiwe ndogo au jiwe la ajabu



Mwishoni, kila kundi kitaonyeshana kwa wengine yale waliyoweza kukusanya.

8. Filimbi katika Msitu



Kuwa na mtoto akiigiza akiwa “mbweha” na kumpa filimbi, ondoka msituni dakika chache kabla ya watoto wengine. Piga filimbi kwa vipindi vifupi ili wengine waweze kuifikia wakiongozwa na sauti. “Mbweha”, kila mara anapiga filimbi, anaweza kupiga katika mwelekeo tofauti. Mbweha akihisi

amefumaniwa, piga filimbi mpaka washirika wote wafike pale alipo. Unaweza kuongeza shughuli tofauti kwa kila hatua ambayo mbweha anakuongoza. Kwa mfano, wanaenda eneo ambalo wanaamini kuwa mbweha anapiga filimbi na kugundua shughuli ya kufanya. Kwa mfano: Ruka juu mara tano, sema fungu muhimu la somo, pipi kwa kila mwanafunzi, au vinywaji kwa kila mtu, nk.

9. Vyombo ya Vijiti

Watoto wanapenda kuweka vijiti na matawi pamoja. Tengeneza chombo rahisi kutoka kwa matawi kavu, ukitumia tepe za mpira ili kuyashikilia katika chombo au kopo tupu. Fanya watoto kukusanya matawi na vijiti vyao, na kuhakikisha kuwa ni virefu zaidi kuliko urefu wa chombo. Weka tepe 2 za mpira kuzunguka chombo hiki na kuweka vijiti chini ya tepe za mpira hadi chombo kiwe kimefunikwa.



Telezesha tepe pamoja na uziweke riboni nzuri. Ikiwa unataka, unaweza kupunguza matawi yote kuwa urefu sawa. Jaza chombo hicho na maua ya mwituni ili kurembesha eneo lako la chakula au kutuma nyumbani kama zawadi kwa familia za wanafunzi wako.

10. Chaki za Kujitengenezea



Fanya wanafunzi wako wafurahie kutengeneza chaki kwa urahisi wakitumia “Plasta ya Paris” !Kila mtoto anahitaji tyubu ya karatasi ya choo, foili ya alumini, sahani ndogo isiyo ya kudumu na kijiko. Pia watahitaji rangi fulani ili kupaka rangi kwenye chaki na utepe .Fanya

wanafunzi wako waanze shughuli kwa kufunika ukingo mmoja wa chupa ya karatasi ya choo na utepe wenye nguvu .Viringisha kipande cha foili ya alumini na kukiweka ndani ya tyubu ili iweze kuingia ndani na kulingana. Weka tyubu kwa wima (utepe ukiangalia chini) kwenye uso uliohifadhiwa. Katika vikombe, wasaidie wanafunzi wako kuchanganya kikombe 1 cha plasta ya Paris na kikombe nusu cha maji. Changanya polepole na kikamilifu hadi mchanganyiko utenguliwe, takriban dakika 1. Mara moja ongeza vijiko 2 vya rangi (au zaidi ili kutoa rangi yenye nguvu kwenye chaki, kuwa makini kwa sababu inaweza kuharibu.) Changanya vizuri. Weka kijiko ndani ya tyubu na kupiga polepole ili mchanganyiko uende chini. Ruhusu ikauka usiku huo kabla ya matumizi.

11. Ufundi wa Chupa ya Maji

Tengeneza chupa zako za maji pamoja na wanafunzi wako wakati wanapokwenda kambini .Patia kila mwanafunzi chupa ya maji isiyo ya kudumu na kitambaa gandamizo au karatasi kwa ajili ya kuipamba. Mapambo rahisi ni kuweka chupa ya maji juu ya kitambaa gandamizo na kuviringisha kitambaa gandamizo juu ya chupa na kutumia gundi ya



silika kuunganisha pamoja. Unaweza kuimarisha sehemu za ukingo kwa kutumia sindano na kamba. Unaweza pia sokota pamoja sehemu za kitambaa ili kutengeneza mpini. Unaweza kutumia gundi ya silika kuunganisha mpini na kuimarisha kwa sindano na kamba.

Ufundi



12. Ufundi wa Sanduku la Barua

Wanafunzi wanaweza kutengeneza masanduku yao ya barua kutoka kwa kopo lenye kifuniko! Kwa njia hii unaweza kupitisha taarifa kati ya kila mmoja mkiwa kambini, kupokea taarifa za ucheshi kutoka nyumbani au kutoka kwa kiongozi wako wa kambini.

Kila mwanafunzi anaweza kupamba anavyopenda sanduku lake la barua, kisha kufunga sanduku mtini, au kuiweka kati ya matawi ya mti. Hebu furaha ianze!

13. Michoro ya Asili

Hii ni wazo rahisi. Kutengeneza “usanifu” au “michoro” hii weka kipande cha karatasi nyeupe kwenye jani la mti au kitu chochote chenye mfumo unaotaka kama gome la mti au nyuso za mawe. Paka krayoni au kipande cha chaki kwenye karatasi (unaweza kutumia chaki uliyotengeneza hapo awali). Sehemu zilizo inuka katika uso zitaleta mistari ya rangi iliyokoza. Baada ya kusugua kidogo, utapata picha ya kitu hicho kwenye karatasi. Watoto wanaweza kutengeneza mikusanyiko ya “usanifu” wakiwa kambini.




14. Mikongojo ya Kutembea



Fanya wanafunzi wako kutafuta mkongojo bora wa kutembea kwa shughuli zao za kutembea. Kuwa na muda wa kuwaruhusu kuipamba. Kuwa na vitu vingine kamibini ili kuwasaidia kupamba; kuongeza uzi wa rangi mbalimbali, manyoya, au shanga. Himiza wanafunzi wako kutumia vitu vwa kiasili kama vile majani ya mti na vijiti vidogo vya kawaida. Watafurahia kutengeneza mikongojo yao, na kuitumia katika matembezi na hata kwenda nayo nyumbani!

15. Kupika kwa machungwa



Keki ya Chokoleti kwa machungwa:

Kata sehemu ya juu ya chungwa - karibu 1/3 chini. Watoto watumie vijiko ili kuondoa sehemu ya ndani ya chungwa - wawe waangalifu wasitoboe au kuathiri ngozi ya chungwa. Kisha andaa baadhi ya mchanganyiko wa keki

Fanya kila mtoto kujaza chungwa lake - karibu 2/3 kamili. Rudisha kifuniko cha chungwa na kuweka chungwa kama limesimama. Funga chungwa kwa karatasi nzito ya alumini (kama inavyoonekana kwenye picha, tabaka

kadhaa itakuwa sawa) na utengeneze tanzi ambayo itasaidia kuondoa machungwa kutoka kwenye makaa kwenye moto wa kambini. Weka machungwa yaliyofungwa kwenye makaa (usiyaweke yakiwa wazi kwenye moto) na kuyafunika hadi uwe na mlima mdogo wa makaa ya moto lakini tanzi iwe nje. Muda wa kupika ni dakika 20 - 25, lakini hii inaweza kuwa tofauti, na inategemea ukubwa wa machungwa na ubora wa makaa - kwa hivyo angalia baada ya dakika 20 ili uone ikiwa iko tayari. Ondoa makaa na kuruhusu alumini iwe baridi kwa dakika chache ili uweze kuigusa - kisha ruhusu watoto kufungua keki iliyookwa ndani ya machungwa - na kula!

Kifungua kinywa ndani ya chungwa:

Chaguo lingine ni kuvunja mayai na kuyachanganya katika bakuli kubwa. Kila mwanafunzi anajaza chungwa lake na mchanganyiko wa yai, anaweka kifuniko na kufunika kwa alumini. Pika juu ya makaa. Weka viungo katika mayai ya machungwa kupata ladha!

16. Ndizi Iliyojazwa

Kwa hili unahitaji ndizi, mashimelo, vipande vidogo vya chokoleti, mananasi membamba au iliyosagwa, jemu ya stroberi, karanga zilizokatwa na foili alumini. (Au chochote unachoweza kupata kwa urahisi katika eneo lako.) Bila kuondoa ngozi ya ndizi, kata mwanya kidogo kwenye ngozi na kufunga viungo pamoja na ndizi katika karatasi ya alumini. Pika kwa makaa.



Vyakula

17. Viazi vilivyopikwa



Funga viazi katika foili ya alumini na uviweke kwenye makaa yanayowaka. Unaweza kuviangalia ukitumia kijiti au uma. Dunga kiasi kwa kijiti au uma. ikiingia kwa urahisi, iko tayari.

Njia nyingine ya kupika ni kuviweka moja kwa moja juu ya makaa yanayowaka au karibu na moto, geuza

mara kwa mara na kuhakikisha havitaungua. Pika bila kuondoa ngozi.

Unaweza pia kuzika: Kwa hili tengeneza moto ndani ya shimo na wakati umewaka, ondoa makaa. Weka viazi kwenye shimo na uzike kwa udongo. Tengeneza moto juu ya shimo lililofunikwa ili kuendelea kupika viazi.

18. Soseji kwa mkate katika kijiti

Andaa mapema kinyunya cha mkate. Wanafunzi wanainua kinyunya na kuwa na mifano ya nyoka wadogo na kuviringisha juu ya soseji. Weka soseji iliyo na kinyunya cha mkate juu yake katika kijiti. Pika kwa moto mpaka kinyunya kiwe tayari. Chakula Kitamu! (Hakikisha utakuwa na viungo.)



19. Mshikaki wa Shish



Kata vipande vya nyama na kuwaacha wanafunzi waviweke kwenye vijiti vya mshikaki pamoja na viungo wanavyopenda. Kuna vitu vingi vya kutengeneza chakula cha jioni chenye ladha kama vile; pilipili za kengele, vitunguu, hoho, nyanya na mananasi. Kwa chaguo za nyama, unaweza kutumia nyama ya nguruwe, kuku, au soseji (hakikisha zimeiva kikamilifu).

20. Mashimelo ya Kuchoma

Usisahau utamaduni wa kuvutia wa kuchoma mashimelo kwenye kijiti. Kuwa tayari na vijiti vingi vya kuchoma na kiasi kikubwa cha makaa karibu na moto. Chunga usiweke mashimelo katika nywele za rafiki yako!

Weka vijiti vyote kwenye mti uliotengwa wa vijiti vya mashimelo ili kuepuka matatizo baadaye.



21. Kuwa na kifaa cha Huduma ya Kwanza



Tafuta sanduku na kujaza kwa vifaa vya matibabu ili kuwa tayari kwa chochote kinachoweza kutokea kwenye kambi yako.

Napendekeza:



* Mikanda ya usafi.



* Krimu kwa ajili ya kuchomwa au Aloe Vera.



* Dawa za kawaida kama vile aspirini au Tylenol ili kupunguza homa.



* Dawa ya jicho ambayo itasaidia ikiwa mtoto ameingiwa na kitu machoni.



* Mbano za kuondoa vivunjo.



* Mafuta ya kuwashwa, kusaidia unapoumwa na mbu na, bila shaka...



* Pepto-Bismol kwa ajili ya kiungulia, tumbo inayouma, kichefuchefu au kuhara.

22. piga kila mtoto picha



Kila wakati piga kila mtoto picha ya hivi karibuni katika kambini yako. Tunatarajia kamwe hautaitumia kwa ajili hii, lakini ikiwa mtoto atapotea, unaweza kutumia picha za hivi karibuni ili kutafuta msaada kwa wengine walio karibu na kambi au kwa utafutaji. Si lazima ziwe nakala halisi za picha - karibu kila mtu siku hizi ana kamera ya digitali na picha iliyo katika simu yako itawezesha kusudi hilo.

Usalama

23. Tangaza sheria za kambi

Chagua sheria unazotaka, lakini hakikisha kila mtu anazifahamu .Jumuisha mojawapo ya vidokezo hivi: Vaa viatu kila wakati, usipigane, hakuna kula ndani ya hema. Na ninayopenda zaidi; tumia mfumo wa “Rafiki”. Hutaki waende sehemu yoyote wakiwa peke yao. Ikiwa huwezi kuwaona, sisitiza waende wakiwa wawili (jinsia sawa).



24. Kuwa makini SANA na tabia za kimapenzi



Wanaume huzingatia huduma zao kwa wanaume na wanawake kwa wanawake. Usiondoke peke yako na mtu wa jinsia tofauti. (Hakuna haja ya kutembea katika misitu na mwanakambi, hata akisema ni kwa kiasi gani anahitaji kuzungumza na wewe.) Usidhani kuwa wengine wanapenda kukumbatiwa nawe au wanataka kuguswa nawe. Na wakati wa kumkumbatia mtu wa jinsia tofauti, kumbatio la muda mfupi ni lile halina “mvurugano”.

25. Kahawa

Hutaki kikundi cha viongozi ambao hawana kahawa ya kutosha katika kambi yako! Kuwa na kahawa au chai kwa wingi kwa watu wote ambao wamekosa usingizi .Hiki ni kidokezo muhimu sana cha usalama, sio tu kwa ajili yako, bali pia kwa wanakambi!



ZIADA ZIADA ZIADA ZIADA ZIADA

Mbio

Mbio ni shughuli iliyopangwa na ina hatua ambazo watoto watatekeleza, kulingana na maelekezo yako. Katika kila sehemu ya mbio, wanapaswa kutafuta njia na kufanya shughuli mbalimbali. Mshindi ndiye atakayefanya shughuli nyingi zaidi au kukusanya idadi kubwa ya vitu. Kila timu inakuja na karatasi ya maagizo na mfuko wa kuweka vitu. Kila kituo kinafaa kusimamiwa na mtu mzima. Rekodi pointi za hatua na kutoa bendera, cheti au kitu kingine.

Mapendekezo:

- * Kula tufaha au mandazi ambayo inaning'inia kwa kamba.
- * Panda mti fulani na kuchukua kitu fulani kama uthibitisho kwamba umepanda, (mfano, bendera).
- * Ruka kamba kwa idadi fulani.
- * Ruka umbali fulani.
- * Panda ngazi ya kamba (unaweza tengeneza mfano wa utando wa buibui au mfano mwingine unaovutia),
- * Rukisha mpira mara kadhaa wakati unaruka juu kwa mguu mmoja.
- * Kuvunja puto kwa kuikalia juu ya kiti.
- * Tafuta vitu vilivyofichwa ndani ya chombo kilichojaa puto (kidibwi cha kujaza hewa kinaweza kutumika kwa lengo hili),
- * Tafuta kitu katika sahani iliyojaa unga. Inaweza kuwa sarafu. Kwa hili, wanapaswa kuchukua wakitumia meno yao huku wameweka mikono yote miwili upande wa nyuma.
- * Tembea juu ya kamba iliyowekwa chini bila kupoteza mwelekeo.
- * Ruka ukiwa ndani ya mfuko, kama gunia, kwa umbali fulani.
- * Ruka kati ya matairi kadhaa yaliyowekwa katika safu mbili.



Jinsi ya kutengeneza hema:




1. Chukua mablanketi kadhaa au shuka na kuzitundikia ili zibaki kwa ukubwa kamili.

2. Tumia viti kufanya hema kuwa imara zaidi. Unaweza pia kutumia madawati, bodi imara au kamba zilizofungwa kwenye miti.

3. Funika fanicha ukitumia mablanketi au shuka. Shikilia sehemu za mwisho wa mablanketi ukitumia vitabu vizito au kuzishikilia ukitumia miguu ya viti. Funga sehemu za mwisho wa mablanketi ili kuongeza eneo lililofunikwa.

4. Weka matakia ndani ya hema kwa starehe zaidi na ufurahie!



Follow us on...

facebook



Like!

ChildrenAreImportant

Camping with
Children Swahili



20165

www.ChildrenAreImportant.com
info@childrenareimportant.com
We are located in Mexico
00-52-592-924-9041

Watoto
ni wa
muhimu